**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu 0768207572**

**Mkuu wa Shule 0755-298756**

**Makamu Mkuu wa Shule 0747783270**

**Matron/Patron 0768207572**

**Shule ya Sekondari MUBABA**

**S.L.P 185, BIHARAMULO**

**Tarehe 02/04/2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MA ELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MUBABA HALMASHAURI YA BIHARAMULO MKOA KAGERA MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 202 4 na atasoma tahasusi ya PCM/PCB/CBG

Shule ya Sekondari Mubaba ipo umbali wa Kilometa 83 Mashariki mwa Mji wa Biharamulo Usafiri wa basi kutoka mjini Biharamulo unapatikana katika kituo cha mabasi Biharamulo Nauli ni Shilingi 7,000 kwa pikipiki na Shilingi 15,000 kwa bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 08/07/2024 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 08/07/2024 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 30/07/2024

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

a) Kwa wasichana - Blauzi/ Mashati mawili meupe ya mikono mifupi yasiyo na urembo wowote.

-  Sketi mbili rangi kijani jeshi za kitambaa cha suruali / suti, zenye marinda manane ya kuzunguka kiuno, ndefu mpaka chini kwenye kiwiko cha mguu..

Kwa wavulana - Mashati mawili meupe ya mikono mifupi

-  Suruali mbili rangi kijani jeshi zenye marinda mawili kila upande, zisiwe na mifuko ya kubandika nyuma au mbele, zisiwe za kubana maarufu kwa jina la (modal). Aidha hakikisha zinavaliwa kiunoni, pia ziwe na pindo chini miguuni, yaani (Turn-up)

b) Rangi ya hijab (kijuba) iwe nyeupe.

c) · Sare ya michezo kwa shule hii ni; T-shirt/Jezi mbili za rangi ya bluu, bukta/Track suit" mbili za rangi ya bluu, raba na soksi / stocking za michezo.

d) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi, viwe vya ngozi.

e) Soksi jozi mbili nyeusi.

f) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi, usiwe na chuma kipana wala urembo wowote.

g) Sweta rangi ya damu ya mzee inapatikana hapa shuleni.

h) Nguo za kushindia "T-shirt" Sare ya shule inapatikana hapa shuleni (kwa wavulana na wasichana). Gauni (shamba dress) Sare ya shule lenye rangi ya pinki linapatikana hapa shuleni (kwa wasichana tu)

- Suruali mbili za rangi "damu ya mzee" yenye sifa kama kwenye kipenge1e (a) Hapo juu, (kwa wavulana tu)

i) Tai rangi kijani jeshi na nyeupe (wote wavulana na wasichana) zinapatikana shuleni.

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari yasiyopungua kumi;
ii. **Ream (A4)** Double A ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha iambatishwe*);
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator;
vi. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni liwe na vipimo kulingana na vipimo vilivyopo katika shule husika.
vii. Mashuka Jozi 2 rangi light blue, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 light blue
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Sabuni ya chooni lita tano(5)
xii. Pia waje na vifaa vifuatavyo kulingana na combination anayosoma

| | | | |
|---|---|---|---|
| PCM | i.Reki 1 | ii.Mopper 1 | iii.Panga |
| PCB | i.Softbroom 1 | ii.Hard brush 1 | iii. Kotama |
| CBG | i.Jembe 1 | ii.Kwanja 1 | iii.Fagio la buibui |

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Michango yote ilipwe kwenye akaunti ya shule NMB 31701200088 jina MUBABA SECONDARY SCHOOL Kumbuka kuandika jina la mwanafunzi kwenye payslip ya kulipia na kidato anachosoma mwanafunzi.

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);

iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;

x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ……………………………………….**

**Jina la Mkuu wa Shule ALFRED SWEYA KATOBESI**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0755298756.**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0747783270**
- **Mwandamizi Taaluma 0768207572**
- **Mwandamizi Malezi 0768207572**